Songea,
20 Septemba, 2026

TAARIFA KWA UMMA

OFISI YA MKUU WA MKOA WA RUVUMA YASIKITISHWA NA UPOTOSHAJI WA TAARIFA KUHUSU UNUNUZI WA BASI LA OFISI YA MKUU WA MKOA

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma imesikitishwa na upotoshaji unaosambazwa mitandaoni kuhusu ununuzi wa gari (basi dogo) aina ya **"Toyota Coaster"** mali ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma.

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa inapenda kujulisha Umma kuwa taarifa zinazosambazwa mitandaoni zimepotosha maudhui ya nia njema ya ununuzi wa gari hilo kwa makusudi kwa kuonesha na kutilia mashaka uhalali na umuhimu wa ununuzi wa gari hilo.

Hivyo Ofisi inajulisha kuwa ununuzi wa gari hilo ulifuata taratibu za ununuzi wa magari ya Serikali kupitia **Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini (GPSA)** ambapo gari hilo lenye usajili STN 7615 limenunuliwa jipya na la kisasa kwa gharama ya Shilingi za kitanzania Milioni 334 likiwa halijatembea (kilometa sifuri - 0 km).

Basi hilo lenye uwezo wa kubeba abiria 30, limenunuliwa maalum kwa ajili ya kuboresha usafiri wa watumishi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma na wadau wa Maendeleo katika Mkoa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za maendeleo za wananchi wa Mkoa wa Ruvuma.

Aidha ununuzi wa gari hilo umelenga kupunguza matumizi ya fedha za Serikali ambapo gari hilo litaweza kuwa mbadala wa matumizi ya magari mawili mpaka matano kwa safari moja ambapo litatumika moja badala ya magari mengi na hivyo kutumia mafuta kidogo na kupunguza uchakavu wa magari madogo.

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa inatoa wito kwa watumiaji wa mitandao ya kijamii, wadau wa habari, Wanahabari na wananchi kwa ujumla kutumia uhuru wa kujieleza kwa kuzingatia ukweli, uhalisia wa jambo ili kuepuka kutoa taharuki kutokana na maneno yenye lengo la kupotosha lengo la ununuzi wa gari hilo.

Hivyo Ofisi inatoa wito kupuuzwa taarifa zinazosambaa mitandaoni zenye nia ya makusudi ya kupotosha ukweli kuhusu ununuzi wa gari hilo. Ofisi itaendelea kusimamia rasilimali za umma kwa uadilifu mkubwa kwa ustawi wa wana-Ruvuma na Taifa kwa ujumla.

Imetolewa na:
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini,
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma.